**KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA**
**K.K.K.T.DAYOSISI MKOANI MARA.**

**USHARIKA WA TARIME**

**SIMU: +255784751822**
**+255768071000**
**+255764732622**

**SHULE YA SEKONDARI SAMARITAN NA UFUNDI**

**S.L.P.33,**
**TARIME.**

**(NAMBA YA USAJILI S. 3884)** **website: https://samaritantechnical.ac.tz**

Kumb.Na. STSS/ADM/APF/VOL.3/5 Tarehe: 20-10-2025

Namba yafomu__________Jina la mwanafunzi______________________________S.L.P________ Shule aliyosoma:______________________Kata:________________Mji/Wilaya______________Mkoa:________

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KWA WANAFUNZI WA BWENI /KUTWA 2026**

**UTANGULIZI:**

**Shule ya Sekondari Samaritan na Ufundi** ilianzishwa mwaka 2008 na imesajiliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa namba ya usajili **S.3884.**

**MAHALI ILIPO:** Shule hii iko Tarime mjini katika Halmashauri ya Mji wa Tarime mtaa wa Samaritan mkabala na Goldland Hotel mita 150 na mita 5 tu kutoka kanisa la K.K.K.T.

**MASOMO:** Shule ni ya mchepuo wa **Sayansi** na **Sanaa**, pia inatoa masomo ya **Ufundi.**

**MASOMO YANAYOFUNDISHWA:**

**MKONDO WA JUMLA**

1. **Basic Mathematics**
2. **English Language**
3. **Kiswahili**
4. **Historia ya Tanzania na maadili**
5. **Geography**
6. **Biology**
7. **Chemistry**
8. **Physics**
9. **Bible knowledge**
10. **Computer science**

**MKONDO WA AMALI**

1. **Graphics and design**
2. **Electrical Installation**
3. **Brick work and Masonry**
4. **Computer programming**
5. **Welding and metal fabrication**

Shule hii ni ya mchanganyiko ( wasichana na wavulana) ambao ni bweni/kutwa na inapokea maombi ya kujiunga na Muhula wa Masomo .2026...... Ambapo itaanza kupokea wanafunzi kwa muhula wa masomo mwaka ..2026..... kuanzia tarehe .05-01-2025... ambapo wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria masomo bila kukosa.

**MAHITAJI MUHIMU:**

(a) **Ada kwa wanafunzi wa Bweni na Kutwa:-**

| | | BWENI | KUTWA BILA USAFIRI | KUTWA NA USAFIRI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Karo | 750,000 | 750,000 | 750,000 |
| 2. | Chakula | 485,000 | 385,000 | 385,000 |
| 3. | Malazi/Usafiri | 200,000 | | 100,000 |
| 4. | Uchakavu | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| 5. | UMISETA | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 6. | TAALUMA | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| 7. | Hudumaya kwanza | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| 8. | Kitambulisho (Identity card) | 5,000 | 5,000 | 5,000 |
| | JUMLA | **1,600,000/=** | **1,300,000/=** | **1,400,000/=** |

(b) **Ada iliyo ainishwa hapa chini, ni kwa wanafunzi wa Kutwa, Bweni na wageni/wanaohamia italipwa kwa awamu tatu kama ilivyokatika jedwali.**

| | Januari | April | Julai | Septemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **KUTWA BILA USAFIRI** | **500,000/=** | **230,000/=** | **330,000/=** | **240,000/=** | **1,300,000/=** |
| **KUTWA NA USAFIRI** | **520,000/=** | **275,000/=** | **330,000/=** | **275,000/=** | **1,400,000/=** |

| | Januari | April | Julai | Septemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **BWENI** | **585,000/=** | **295,000/=** | **420,000/=** | **300,000/=** | **1,600,000/=** |

**(c). Kwa wanafunzi wanaoendelea watalipa ada kama ifuatavyo kwenye jedwali.**

| | Januari | April | Julai | Septemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **BWENI** | **570,000/=** | **300,000/=** | **420,000/=** | **260,000/=** | **1,550,000/=** |

| | Januari | April | Julai | Septemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **KUTWA BILA USAFIRI** | **420,000/=** | **240,000/=** | **350,000/=** | **240,000/=** | **1,250,000/=** |
| **KUTWA NA USAFIRI** | **450,000/=** | **275,000/=** | **350,000/=** | **275,000/=** | **1,350,000/=** |

**Malipo yote yatafanywa kupitia akaunti za shule na Mhasibu wa shule atapokea Bank Pay – in slip na sio vinginevyo: HATUPOKEI PESA TASLIMU**

**AKAUNTI ZA SHULE:**

1. **CRDB BRANCH. 0150042362900 ( SAMARITAN TECH. SEC. SCHOOL)**
2. **NMB BRANCH. 30406600087 (SAMARITAN TECH. SEC. SCHOOL)**

**(d). <u>SARE ZA SHULE:</u>**

(i). **Wavulana:**

1. Surual imoja (01) Kijani nyeusi **(Dark green)** **(inapatikana shule Bure**).
2. Suruali moja (01) Nyeusi (**Black**) **(kwa wanafunzi wa bweni tu)** ( **inapatikana shule Bure**).
3. Suruali moja (01) Bluu nyeusi **(Dark bluu)** **(inapatikana shule Bure**).
4. Sweta (02) kijani nyeusi (**Dark green**) (**Nunua**)
5. Shati mbili (02) Nyeupe za mikonomifupi. (**Nunua**)
6. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi mbili. (**Nunua**)
7. Soksi nyeupe jozi mbili. ( **Nunua** )
8. Tai mbili (02) moja ya kijani nyeusi na nyingine iwe ya bluu nyeusi. ( **zinapatikana shule bure**).
9. Bukta na T – shirt za bluu (rangi ya Chelsea) kwa ajili ya michezo. (**Nunua** )
10. Raba jozi moja kwa ajili ya michezo. (**Nunua** )
11. Mikanda miwili rangi nyeusi kwa ajili ya kuvalia suruali. ( **Nunua**)
12. Rimu mbili karatasi **(Double A) A4** kwa kidato cha kwanza (**Nunua)**
13. **Track suit ya Bluu ( rangi ya chelsea**), **T – Shirt ya bluu**, na **kaptula ya Bluu** kwa ajili ya michezo na mazoezi.
14. **T-SHIT** mbili za damu ya mzee zenye colar (**Zinapatikana Shuleni Bure**)

(ii). **Wasichana:-**

1. Sketi moja (01) kijani nyeusi **(Dark green).** ( **Zinapatikana Shuleni Bure**).
2. Sketi moja (01) Nyeusi **(Black)(kwa wanafunzi wa bweni tu)( Zinapatikana Shuleni Bure)**

3. Sketi moja (01) Bluu nyeusi **(Dark bluu).** ( **Zinapatikana Shuleni Bure**).
4. Shati mbili (02) nyeupe mikono mifupi. ( **Nunua**)
5. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi mbili. ( **Nunua**)
6. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili. ( **Nunua**)
7. Sweta (02) kijani nyeusi **(Dark green)** **(Nunua)**
8. Tai mbili (02) moja ya kijani nyeusi na nyingine iwe ya bluu nyeusi.( **Zinapatikana Shuleni Bure**)
9. **Track suti rangi ya Bluu (Chelsea) na T – shirt ya bluu (Chelsea)** kwa ajili ya michezo na mazoezi. ( **Nunua**
10. Raba jozi moja kwa ajili ya michezo na mazoezi. ( **Nunua**)
11. Njoo na Rimu mbili (02) karatasi (**Double A**) A4 ( **Nunua** )

## MAHITAJI MENGINEYO:

- Kwa wanafunzi wa Bweni wanatakiwa kuja na Shuka mbili rangi ya **bluu** kwa *wavulana* na rangi ya **pink** kwa *wasichana*, **mashuka mengine kama vile shuka za Maasai na shuka za rangi nyingine ni marufuku hapa shuleni**, blanketi, Chandarua 3½ x 6, Mto wa kulalia na foronya mbili, Taulo moja, ndoo ndogo kwa ajili ya kuogea na kufulia, Kontena la chakula lenye mfuniko – la plastiki, kikombe, Kijiko, Sabuni, Dawa yameno, kopo la kubebea maji ya kunywa, toilet paper. Kiwi, Brush, Kandambili, Kitana cha nywelena Mafuta yakujipaka yasiyokuwa na kemikali (**Mkorogo).**
- **Scientific calculator kwa kidato cha kwanza hadi cha nne (zinapatikana shuleni kwa gharama ya 28,000= tu.**

- Kila mwanafunzi aje na fyekeo na ndoo ya lita 20 kwa ajili ya usafi wa mazingira ya shule, counter books 12, Mathematical set (**NATARAJ**) na mfuko wa kubebea vitabu/madaftari.

- Aje na daftari ndogo aina ya msomi 12 kwaajili ya mazoezi Pamoja na **graph pad 2**

- Kila mwanafunzi anatakiwa aje na saa ya mkononi ya bei nafuu .
- Mwanafunzi aje na SQUIZER MOJA ( MOPPER) na mfagio mmoja (chelewa)
- Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na Dictionary yakiingereza ndogo aina ya OXFORD, na vitabu vya masomo atakayosoma.
- Aje na jembe 1 na mpini wake

**N:B:**

1. **Kwa kidato cha kwanza – sare na Godoro vinapatikana shuleni bure.**
2. **Pesa ya kunyolea kwa mwaka Tshs. 10,000/= (Kwa mwanafunzi wa bweni tu).**
3. **Hela ya ziara ya masomo Tsh 100,000/= ni lazima kwa kidato cha kwanza na kidato cha tatu tu.**
4. **Wanafunzi wanaohamia kidato cha II, III na IV waje na magodoro yao na biblia moja ya kiingereza**
5. **Kwa wavulana sare zinapatikana shule kwa Tsh. 85,000/= Na wasichana sare zinapatikana shuleni kwa Tsh. 92,000/=**
6. **Nakala ya cheti cha kuzaliwa**

## SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

**Shule ya Sekondari na Ufundi Samaritan** ni shule inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (K.K.K.T) Dayosisi Mkoani Mara Usharika wa Tarime Kati. Hivyo basi mwanafunzi anayejiunga na shule hii anapaswa kufuata taratibu na maadili ya shule kama ifuatavyo:-

1. Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria **Ibada kila siku** kwa kuzingatia ratiba ya shule bila kukosa.
2. Mwanafunzi anapaswa kusoma kwa bidi na kuhakikisha kwamba anamudu wastani wa shule ambao ni *55%. Mwanafunzi asipofikisha wastani unaohitajika atalazimika kukariri darasa au Mzazi atalazimika kumhamishia mtoto shule nyingine*. Kwa vidato vya mitihani wanafunzi watapewa mitihani ilikupima uwezo wao kabla ya kuwasajili.
3. Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vi pindi vyote darasani bila kukosa.
4. Mwanafunzi kujiamulia kufanya jambo la aina yoyote ile bila maelekezo yoyote ni kinyume na utaratibu wa shule.
5. Kama taasisi ya kidini mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na ulevi, kufuga kucha, nywele, ndevu, kuvaa mavazi yasiyo ya heshima, kuiga mitindo ya kihuni, kujiremba na kuhudhuria kumbi za muziki au sehemu mbalimbali za starehe.
6. Mwanafunzi wa shule ya **Sekondari na Ufundi Samaritan** anapaswa kuwa msafi muda wote na mwenye nidhamu kwa wa kubwa na wadogo.
7. Kila mwanafunzi awapo shuleni anapaswa kutumia lugha ya Kiingereza kwa mawasiliano kwa muda wote atakaokuwa ndani ya eneo la shule.
8. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi shuleni.

## YAFUATAYO NI MAKOSA YANAYOMWONDOA MWANAFUNZI MARA MOJA SHULENI:-

1. Kuharibu/kuiba mali ya wanafunzi wenzako.
2. Lugha ya kiingereza inatumika kwa mawasiliano wakati wote katika eneo la shule. Kutoitumia itamuondoa mara moja shuleni.
3. Wizi wa aina yoyote ile.
4. Mwanafunzi kujihusisha na Uasherati, Ubakaji, Ushoga, Usagaji na ulevi (pombe, madawa ya kulevya kama kubeli, mirungi, bangi, cocaine).
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
9. Kuoa ama kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba au kushiriki kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama ndani ya shule au Nje ya shule.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Utoro uliokithiri.
15. Kutohudhuria Ibada.
16. Kuondoka ndani ya eneo la shule bila ruhusa (mfano kuruka uzio wa shule na Kwenda nje ya eneo la shule).
17. Kuwa na simu ya mkononi shuleni, kamera au redio shuleni.
18. Udanganyifu katika mitihani yoyote hapa shuleni.
19. Kuja shuleni na silaha ya aina yoyote (panga, kisu, rungu, sime, n.k).

## MWONGOZO WA SHULE:

Shule kama kiwanda ni mahali pa kuandaa wataalamu watakaoliongoza Taifa katika Nyanja mbalimbali za kitaaluma kwa siku za baadaye. Maandalizi hayo yanahitaji juhudi za Pamoja baina ya mwanafunzi kutambua kuwa anakuja kupambana na kazi ngumu inayomtaka ajitoe kikamilifu na kujinyima mengi. Kwa mantiki hiyo hatutegemei mwanafunzi kujiingiza kwenye mambo yaanasa. Shule haitavumilia mwanafunzi mzembe anayetoa visingizio vya kutofanya kazi ndani na nje ya darasa. Wanafunzi wenye matatizo ya kiafya wajulikane tangu mwanzo kupitia kwa Daktari wa hospitali ya Serikali.

**Hatutakubaliana na maelezo ya mdomo kuhusu matatizo ya kiafya ya mwanafunzi, Mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya ni vyema apate matibabu kabla ya kujiunga na Shule, kama niugonjwa usiotibika tupate taarifa kwa maandishi kutoka kwa Daktari.**

## MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUFANYA:

1. Kufuata taratibu zote kama zilivyooneshwa katika ratiba ya Shule na kama zitakavyokuwa zinatolewa na Uongozi wa Shule mara kwa mara.
2. Kuwa na utii na heshima kwa wafanyakazi wote wa Shule, viongozi na raia wotekwaujumla wake.
3. Kuheshimu Bendera, wimbo wa Taifa na alama maalumu za Kitaifa.
4. Kulinda maadili yaliyo katika **KAULI – MBIU** ya Shule yaani ***Elimu kwa wote na wote kwa Mungu.***
5. Kutumia Kiingereza daima wakati wote wasaa za masomo na kwa kuwasiliana ndani ya mazingira ya Shule.
6. Kuzingatia usafi na hifadhi ya mazingira wakati wote na kilamahali anapokuwa.
7. Kushiriki kutathmini na kuheshimu kazi zote zinazotolewa na Uongozi wa Shule.
8. Kuhudhuria Shule na vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa kadiri inavyompasa.
9. Kuzingatia ahadi hii ***"nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu na kutumia elimu yangu kwa faida ya wote"***

## TAREHE YA KUFUNGUA SHULE.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza ***tarehe***..05-01-2026..........Mwanafunzi atatakiwa kufika shuleni muda uliopangwa saa 02:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni. Mara mwanafunzi afikapo atatakiwa kuripoti Ofisi ya **MKUU WA SHULE** kwa mapokezi na kusajiliwa na **MHASIBU WA SHULE** atahakikisha kuwa Mwanafunzi amekuja na mahitaji kamili ya fedha na vifaa vyote alivyoagizwa katika barua hii, vinginevyo hatapokelewa.

## AHADI YA MWANAFUNZI/MZAZI/MLEZI KUSHIRIKIANA NA UONGOZI WA SHULE:

**KWA MWANAFUNZI:**
**Nimesoma na kukubaliana na taratibu zote za shule na nina ahidi kutekeleza.**
Jina.......................................................................Sahihi..................................Ta
e ......................

**KWA MZAZI/MLEZI:**
Nimesoma na kuafiki taratibu zote za shule na ninaahidi kushirikiana na Uongozi wa shule katika malezi ya mtoto.

Jina....................................................................... Sahihi..............................
Tarehe.....................

## AHADI YA MZAZI/MLEZI YA KULIPA KARO NA MICHANGO YA SHULE.

**Uthibithisho wa Mzazi /mlezi wa kulipa karo na michango ya shule:-**

Mimi ......................................................mzazi/mlezi wa
mwanafunzi...............................................
Anayesoma kidato cha ......... katika **Shule ya Sekondari Samaritan na Ufundi**. Nathibithisha kuwa nipo tayari kulipa karo kama inavyooneshwa kwenye fomu ya maelekezo na kwamba niko tayari kushirikiana na Uongozi wa Shule katika kusimamia malezi na makuzi ya mwanafunzi kwa hali na mali. Sambamba na hilo nitakubali kulipa michango yote itakayoidhinishwa na Bodi ya Shule au Kamishna wa Elimu kadiri ya maelekezo kwa ajili ya

kusimamia na kufanikisha maendeleo bora ya utoaji elimu husika. **Aidha ninaahidi kuwa nitafany amalipo ya ada kwa wakati kama ilivyoelekezwa na shule.**

Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………….. S.L.P …………Mji………………… Namba ya simu………………………………………………
Sahihi ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………….
Tarehe………………………………

## URAIA WA MWANAFUNZI.

Mwanfunzi anatakiwa kuripoti Shuleni na hati ya kuzaliwa (***Birth Certificate)*** ama hati ya kiapo (***Affidavit Form)*** iliyosainiwa na mahakama inayotambulika kisheria.

## HISTORIA YA MWANAFUNZI.

1. Jina la mwanafunzi …………………………..………… Tarehe ya kuzaliwa ……………..………
2. Jina la mzazi/mlezi ……………………………………….………………………...
3. Kama nimlezi: uhusiano…………………………………………………..……….
4. Anuani ya kudumu ya mzazi/mlezi.:………….……..……Simu namba………………….……….
5. Mahali alipozaliwa: kijiji cha………..Kata ya…………..…Tarafa ya …………... Wilaya ….....................
6. Dini…………………..………dhehebu…………..……………………
7. Ame ingia kidato cha ………………. tarehe/mwaka ……………………………………………
8. Ndugu wengine ambao wanaweza kupelekewa Habari muhimu juu yako/maswala ya shuleni :
   i) ……………………..……………………..uhusiano……….……….simu…………...............
   ii) ………………………..……………………..uhusiano……………… Simu …………………...
   iii) ……………………….……………………uhusiano…………….….. Simu …………………

**Hao waliotajwa hapo juu ndio wanaruhusiwa kuja kumtembelea mwanafunzi hapa shuleni.**

9. Kabla ya kuja hapa umepimwa na mganga?................ Ni ugonjwa upi ambao ni wa kudumu kwako? Sifa maalum ……………………..……………………………..

## HITIMISHO.

**"ELIMU KWA WOTE NA WOTE KWA MUNGU"** ni kaulimbiu ya maisha bora na endelevu kwa maendeleo ya Taifa, hivyo shule inahitaji nidhamu, utii na ushirikiano toka kwa mwanafunzi, mzazi na Uongozi wa shule kwa ujumla ili kuweza kupata mafanikio bora katika makuzi yake kitaaluma na kiroho pia.

***NB: Siku za kusalimia wanafunzi ni***

1. ***Jumamosi ya mwisho wa pili***
2. ***Jumamosi ya mwisho wa mwezi wa nane na***
3. ***Jumamosi ya mwisho wa mwezi wa kumi pekee***

***ZINGATIA HILO***

***Tafadhali fika ofisi ya walimu kwanza ili upate maelekezo, zaidi***
***Aidha unashauriwa kufuatilia maendeleo ya kitaaluma, kinidhamu na kiroho ya mwanao kila mwezi***

**"ELIMU KWA WOTE NA WOTE KWA MUNGU"**

THE HEADMASTER
SAMARITAN TECH. SEC. SCHOOL
P.O. BOX 33 TARIME.

…………………………………
**ABDUL JOSEPH**
MKUU WA SHULE

EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA
E.L.C.T. DIOCESE IN MARA REGION

TARIME PARISH
PHONE: +255784751822
+255768071000
Email. Samaritan411@gmail.com

SAMARITAN TECHNICAL
SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 33 – TARIME
**https://samaritantechnical.ac.tz**

**(Regd.S.3884)**

## MEDICAL EXAMINATION.

Students full Name: ........................................Sex:..........................Form ................

Age ........................... height (In cm)........................................
Weight........................

1. Blood count...........................................................................................
2. Stool Examination....................................................................................
3. Urine analysis.........................................................................................
4. Syphilis and other V.D.R.L......................................................................
5. T.B. and Leprosy Test ............................................................................
6. Eye test ..............................................................................
7. Ears test ...............................................................................................
8. P.U.D Test ............................................................................................
9. Abdominal Test ......................................................................................
10. Plano Test ............................................................................................
11. Spleen ..................................................................................................
12. Asthma ..............................................................................................

Additional information e.g. physical defects or impairments infection chronic of family Disease (e.g. sickle cells) inability to eat certain food etc.
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
....................

I certify that the above student is fit/ is not fit to pursue Secondary Education.

Signature.......................................................................
Designation....................................................................
Station............................................................................
Date ...............................................................................